

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

**Simu:** +255-26-2323189

**Barua** pepe:  
[ps@moha.go.tz](mailto:ps@moha.go.tz)

**Tovuti:** [www.moha.go.tz](http://www.moha.go.tz)



Mji wa Serikali - Mtumba,  
Mtaa wa Habari/Afya

S. L. P. 2916,  
40483 DODOMA.

*Unapojibu tafadhali taja:*

14 Novemba, 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

**ZOEZI LA UHAKIKI NA UHUISHAJI WA TAASISI ZA KIDINI ZILIZOSAJILIWA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KUANZA TAREHE 21 NOVEMBA 2022  
HADI MACHI 2023**

Ofisi ya Msajili wa Jumuiya, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, itaendesha Zoezi la Uhakiki na Uhuishaji wa Vyeti vya Usajili wa Taasisi zote za Dini zilizosajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Zoezi hili litaendeshwa katika Kanda saba kuanzia tarehe 21 Novemba 2022 hadi mwezi Machi 2023.

Zoezi hili litaanzia katika Kanda ya Mashariki inayohusisha Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, kuanzia tarehe 21 Novemba 2022 hadi tarehe 3 Desemba 2022. Ratiba ya Zoezi katika Kanda nyingine itatangazwa baadae, Aidha zoezi hili litaendelea kufanyika katika Ofisi ya Msajili iliyopo jijini Dodoma katika kipindi chote cha Zoezi.

Viongozi wa taasisi za kidini wanasisitizwa kufika kwenye Kituo cha Kuhakiki na Kuhuisha Vyeti vya Usajili, wakiwa na :

- Cheti cha Usajili pamoja na Nakala ya Cheti hicho,
- Katiba na Kanuni zinazotumiwa na Jumuiya kwa sasa,
- Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Miaka mitano iliyopita,
- Taarifa ya Utendaji kwa kipindi cha Miaka mitano iliyopita,
- Uthibitisho wa Malipo ya Ada kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, pamoja na
- Ada ya shilingi 100,000/= kwa ajili ya kupatiwa Cheti kipya.

Taasisi za Kidini zitakazoshindwa kushiriki katika zoezi hili zitahesabika kuwa hazipo hai na hivyo taratibu za kufuta usajili wake na kuondolewa kwenye Rejista ya Usajili zitachukuliwa.

Taasisi za Kidini zilizopo Mikoa tajwa zitakazohitaji Huduma yoyote ya Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ikiwemo Ulipaji wa Ada ya Mwaka na kuwasilisha Maombi ya Usajili kwa taasisi zisizosajiliwa, zitapatiwa huduma hizo kwenye Kituo cha uhakiki na uhuishaji wa vyeti vya usajili.

Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi wasiliana na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kupitia namba ya simu +255734712744, +255734712745 au barua pepe [rs@moha.go.tz](mailto:rs@moha.go.tz).

Imetolewa na:

**MSAJILI WA JUMUIYA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**